# DIBAJI

Kuna wakati katika maisha ya mwanadamu ambapo kelele za dunia hupungua polepole,na ndani ya kimya hicho cha ajabu huanza kusikika maswali ambayo hayaji kwa ajili ya kujibiwa haraka,bali kwa ajili ya kuyaishi,kutafakariwa na kueleweka hatua kwa hatua kupitia safari ya maisha yenyewe.

Swali la **“Mungu ni nani?”** ni mojawapo ya maswali hayo,sio swali la akili pekee bali la moyo,roho na uzoefu wa ndani wa mwanadamu,ni swali ambalo halijawahi kumalizika,kwa sababu kila kizazi hulijibu kwa lugha yake,kila mtu hulihisi kwa namna yake na kila moyo hulitafsiri kulingana na safari yake binafsi.

Kitabu hiki cha **“mungu halisi”** kimeandikwa kutoka katika nafasi ya tafakari ya kina,si kama mamlaka ya mwisho ya ukweli,bali kama mwanga mdogo unaowekwa kando ya njia ya msafiri.

Hili ni jaribio la kuangalia upya yale ambayo mara nyingi tumeyachukulia kama ya kawaida na kujaribu kuyatazama kwa macho mapya ya ndani ya utulivu zaidi.

Katika ulimwengu wa leo,watu wengi wamezoea kupokea majibu kabla hata ya kujiuliza maswali,tumefundishwa kuamini haraka,kuhukumu haraka na wakati mwingine kukataa bila kuchunguza,lakini maisha ya kiroho hayakui kwa haraka hivyo uelewa wa kina huota taratibu,kama mbegu inayohitaji udongo,maji na muda wa kukua kabla haijawa mti.

Hivyo basi kitabu hiki hakikuandikwa kukulazimisha uamini jambo fulani,bali kukualika utafakari,kukualika ukae na maswali bila kuyakimbia,kukualika uangalie ndani yako na kuangalia maisha yanayokuzunguka kwa jicho la upya.

Katika kurasa hizi,tutagusa dhana ya mungu si kama wazo lililofungwa katika mfumo mmoja,bali kama uhai unaojidhihirisha katika maumivu,katika ukimya,msamaha,uzuri wa asili na katika nguvu isiyoonekana lakini inayoendelea kuongoza maisha ya mwanadamu kwa njia za ajabu.

Tunapogusa pia katika dhana za dini,si kwa lengo la kupinga,bali kuielewa kama moja ya njia ambazo mwanadamu ametumia kujaribu kile kisichoelezeka kwa urahisi.
Lakini zaidi ya yote,tutajaribu kuangalia kile kilicho nyuma ya maneno,nyuma ya mila na nyuma ya tafsiri zote kile kinachoweza kuitwa uzoefu wa moja kwa moja wa uhai wenyewe.

Ni muhimu kuelewa kuwa kitabu hiki hakidai kumiliki ukweli wote,hakina lengo la kufunga mjadala,bali kufungua milango zaidi ya tafakari,kwa sababu ukweli wa kina hauishi katika hitimisho moja,kuishi katika safari endelevu ya kujifunza,kusahihisha na kuamka upya mara kwa mara.

Kila msomaji anaalikwa kuingia katika kitabu hiki si kama msikilizaji tu,bali kama mshiriki hai wa safari hii,chukua kile kinachogusa moyo wako na acha kile kisichokubaliana na uelewa wako wa sasa,na zaidi ya yote endelea kuuliza maswali yako binafsi kwa uaminifu na ujasiri.

Kwa sababu mara nyingi,majibu tunayoyatafuta tayari yameanza kuota ndani yetu kimyakimya,yakisubiri tu kutambuliwa.

Katika msingi wake **“MUNGU HALISI”** ni mwaliko wa kurudi ndani si kukimbia dunia,bali kuiona kwa kina zaidi,si kupinga maisha,bali kuyaelewa kwa upana zaidi,na si kutafuta mungu kama kitu kilicho mbali,bali kujifunza kuona uwepo wake katika kila pumzi ya sasa.

**KARIBU KATIKA SAFARI HII YA NDANI.**